## Athari za Dawa za Kulevya

Mihadarati ni kitu chochote ambacho hufanya akili ififie au ife ganzi kwa muda na wakati mwingine kumkosesha mtu hisia punde tu kiingizwapo mwilini. Dawa hizi za kulevya zinaweza kuleta **uraibu** zinapotumiwa kwa muda mrefu. Baadhi ya dawa hizi ni kama vile mairungi, kokeini, marijuana, bangi, gundi, sigareti na pombe. Dawa hizi zinaweza kuingizwa mwilini kwa kutumia mbinu ainati kama vile **kumezwa**, **kunywewa**, **kunuswa**, **kudungwa** kwa sindano na sirinji, **kuchanganywa** na chakula miongoni mwa njia nyinginezo. Dawa hizi zina madhara chungu nzima kwa mtumiaji, jamii na taifa kwa jumla.

Ni nani asiyeelewa kuwa mchuma janga hula na wa kwao? Naam, mihadarati imewasababishia watumiaji balaa kwa sababu wao **hutumia pesa nyingi** kununua dawa hizi. Kadiri wanavyoendelea kuzitumia ndivyo akiba yao inavyozidi kupungua. Hatimaye, wao hujikuta wafilisi wasio na mbele wala nyuma.

Fauka ya hayo, dawa hizi husababisha maradhi mbalimbali. Kwa mfano, sigara huweza kusababisha **saratani** ya midomo, koo na mapafu. Tujuavyo maradhi haya humguguna mtumiaji jinsi mchwa wagugunavyo gogo. Navyo vileo kama vile tembo husababisha saratani ya ini, **shinikizo la damu** na **mshtuko wa moyo**. Watumiaji wengine wa mihadarati **hurukwa na akili** na kuwa wehu. Pia, wengine hulazimika kujiingiza katika visa vya uhalifu kama vile wizi ili waweze kugharimia dawa hizi. Wengine hutiwa mbaroni na kula kalenda kutokana na matendo ya uhalifu.

Isitoshe, baadhi ya ajali husababishwa na madereva waliotumia dawa za kulevya. Ajali kama hizi huwasababishia wengi **ulemavu** ambao hawakuzaliwa nao. Wakati mwingine, wengine huaga dunia.

Aidha, serikali hutumia hela nyingi kwa matibabu ya wagonjwa walioathiriwa na mihadarati. Pesa nyingi hutumika kuanzisha vituo vya ushauri-nasaha kwa waraibu wa mihadarati. Vilevile, fedha ambazo wananchi wangezitumia kuanzisha biashara hutumika kununulia dawa hizi.

Hakika, mihadarati ina athari chungu nzima. Wenzangu, tusiwe bendera ambayo hufuata upepo. Tujiepushe na janga hili ambalo linatukodolea macho. Tuzingatie ya wahenga kuwa kinga ni bora kuliko tiba.